

ZIJUE HAKI ZA MSINGI ZA WAFANYAKAZI KWA MUJIBU WA SHERIA MPYA ZA KAZI NAMBA

1.0 UTANGULIZI

Lengo la Makala hii ni kuwawezesha Wafanyakazi Wanachama wa RAAWU kuzifahamu haki zao za msingi pindi wawapo kazini na wakati ajira zao zinapokoma. Ufafanuzi wa sheria hizi unazingatia sheria hiyo ya Ajira na Mahusiano Kazini (Employment and Labour Relation Act, No. 6, 2004). RAAWU kama Chama cha Wafanyakazi kina jukumu vilevile la kuelimisha Wanachama wake ili waweze kufahamu haki zao za msingi wawapo kazini na namna ya kutatua matatizo yasiyo na lazima katika sehemu zao za kazi.

2.0 HAKI YA KUTOSHURUTISHWA KUFANYA KAZI

Mtu yeyote anayeshurutisha mtu kufanya kazi anafanya kosa. Ni haki ya kila mfanyakazi kufanya kazi bila kushurutishwa. Kazi za shuruti ni zile anazopata mtu zikiambatana na vitisho vya adhabu na bila ridhaa ya mhusika. Kazi zifuatazo hazihesabiki kama ni za shuruti.

- a) Kazi yoyote ile chini ya sheria za ulinzi za mwaka 1996.
- b) Kazi ambazo ni sehemu ya kawaida ya majukumu ya kiraia.
- c) Kazi zozote zinazoamriwa kufanywa na mtu aliyehukumiwa na mahakama.
- d) Kazi zozote zinazoamriwa kufanywa wakati wa majanga au hali ya hatari.
- e) Kazi ndogondogo za kijamii.

3.0 HAKI YA KUTOBAGULIWA

Kila mfanyakazi anayo haki ya kutobaguliwa katika ajira, ujira au aina yoyote ya kazi kwa misingi ifuatayo:-

- a) Rangi
- b) Utaifa
- c) Kabila au sehemu ya asili
- d) Mbari (race)
- e) Maoni ya kisiasa au dini

- f) Jinsi
- g) Jinsia
- h) Ujauzito
- i) Ulemavu
- j) Ukimwi
- k) Hadhi kindoa au Majukumu ya kifamilia
- l) Asili ya mtu (Social origin)
- m) Umri
- n) Unyanyasaji
- o) Hali ya maisha
- p) Utaifa wa asili (National Extraction)

4.0 HAKI YA KUJIUNGA

Kila mfanyakazi ana haki ya kujiunga na kushiriki katika shughuli halali za Chama cha Wafanyakazi.

5.0 HAKI YA KUPATA TAARIFA

Mfanyakazi ana haki ya kupewa kumbukumbu ya maandishi ya ajira yake yenye maelezo yafuatayo:-

- f) Jina, Umri, anwani na jinsi yake
- g) Mahali alipoajiriwa
- h) Kazi alizofanya
- i) Tarehe ya kuanza kazi
- j) Aina na muda wa Mkataba
- k) Kituo cha kazi
- l) Saa za kazi
- m) Ujira na vigezo vilivyotumika kukokotoa ujira na maelezo ya marupurupu au malipo ya aina nyingine yoyote na
- n) Maelezo mengine yoyote yanayoendana na kazi

Mfanyakazi ana haki ya kushauriana na mwajiri pale ambapo maelezo ya ajira yanabadilika na kupewa taarifa ya maandishi kuhusiana na mabadiliko.

6.0 SAA ZA KAZI

Kila mfanyakazi ana haki ya kutofanyishwa kazi zaidi ya saa 12 kwa siku. Mfanyakazi ana haki ya kufanyakazi saa za kazi za kawaida zifuatazo:-

- a) Siku sita kwa juma (week)
- b) Masaa 45 kwa juma (week)
- c) Saa 9 kwa siku

Mfanyakazi ana haki ya kutofanya kazi saa za ziada isipokuwa

- Kama kuna makubaliano
- Saa za ziada si zaidi ya saa 50 katika mzunguko wa wiki

7.1 Kazi za Usiku

Mfanyakazi mjamzito ana haki ya kutofanyishwa kazi za usiku:

- Miezi miwili kabla ya tarehe anayetarajia kujifungua au
- Miezi miwili kuisha baada ya kujifungua

Mfanyakazi anayenyonyesha ana haki ya kutofanya kazi usiku

- Baada ya miezi miwili iwapo ana cheti cha daktari kinachothibitisha hawezi kufanya kazi za usiku.
- Mfanyakazi mwenye umri chini ya miaka 18 ana haki za kutofanya kazi za usiku
- Mfanyakazi mwenye cheti cha daktari kinachothibitisha hawezi kufanya kazi usiku ana haki ya kutokufanya kazi usiku.

Mfanyakazi anayefanya kazi usiku ana haki ya kulipwa 5% ya mshahara wake kwa saa kwa kila saa atakayofanya kazi usiku, na iwapo saa atakazofanya kazi ni saa za ziada atalipwa asilimia tano ya kiwango cha saa za ziada.

8.0 HAKI YA KUPUMZIKA

Mfanyakazi ana haki ya kupata mapumziko kama ifuatayo:-

- Dakika 60 iwapo atafanya kazi saa 5 mfululizo.
- Angalau saa 12 mfululizo tangu muda aliomaliza kazi na muda anaotarajia kurudi kuanza kazi.
- Angalau saa 24 mfululizo katika wiki tangu siku atakayomaliza kazi hadi siku atakayoanza kazi.
- Mfanyakazi ana haki ya kulipwa iwapo atatakiwa kufanya kazi wakati wa mapumziko.

- Mfanyakazi ana haki ya kulipwa mara mbili ya mshahara wake wa kila saa atakayofanya kazi siku za sikukuu za kitaifa.

9.0 UJIRA

Mfanyakazi ana haki ya kulipwa kwa kazi aliyoifanya

- a) Wakati wa saa za kawaida mahali pa kazi na katika siku iliyokubaliwa kwa pesa taslim iwapo atakubali alipwe kwa:-
 - i. Hundi
 - ii. Kuingizwa kwenye akaunti yake aliyoichagua kwa maandishi
 - iii. Malipo yakifanyika kwa pesa taslim au hundi lazima yawekwe kwenye bahasha
- b) Mfanyakazi ana haki ya kutokatwa mshahara wake isipokuwa:-
 - i. Makato ni ya kisheria, yanatokana na makubaliano ya pamoja, amri ya Mahakama ya TUZO ya uamuzi au
 - ii. Mfanyakazi amekubali kwa maandishi kukatwa kwa ajili ya kulipa deni

10.0 LIKIZO YA MWAKA

- Mfanyakazi ana haki ya kupata likizo ya siku 28 mfululizo katika mzunguko wa likizo miezi 12
- Mfanyakazi ana haki ya kukataa au kutofanya kazi wakati yupo likizo ya mwaka

11.0 LIKIZO YA UGONJWA

Mfanyakazi ana haki ya kupata likizo ya ugonjwa ya angalau siku 126 katika mzunguko wa likizo kwa miezi 36.

- a) Siku 63 kwa mshahara kamili
- b) Siku 63 kwa nusu mshahara, baada ya kutoa uthibitisho wa daktari.